Jumiko la Maliasili Tanzania

Tanzania Natural Resource Forum

***HABARI JUU YA WANYAMAPORI KATIKA TANZANIA***

**Wanyamapori kwa watanzania wote: Kusimamisha upotevu, kuendeleza raslimali na kupanua mafao**

# CHAPISHO NA. 4

## USIMAMIZI WA WANYAMAPORI NA KUPUNGUZA UMASIKINI

**MASUALA MUHIMU:**

⇨ Wanyamapori wangeweza kutoa mchango mkubwa kisheria katika kupunguza umaskini na kukuza uchumi wa jamii zinazoishi katika maeneo yenye wanyamapori.

⇨ Kwa sasa wanyamapori wana thamani katika jamii zinazofaidika na biashara haramu ya wanyamapori.

⇨ Maendeleo katika kuendeleza usimamizi wa kijamii wa wanyamapori kupitia maeneo ya hifadhi za jamii umekuwa wa polepole na aghali.

⇨ Haki zote za kusimamia na kufaidika kutokana na wanyamapori zinahitaji kurudishwa katika ngazi ya jamii mapema iwezekanavyo ili kutoa motisha chanya juu ya usimamizi endelevu wa wanyamapori miongoni mwa vijiji vinavyopatika na kando ya wanyamapori.

⇨ Kama wanyamapori hawataonesha nafasi katika kupunguza umaskini na kukuza uchumi wa jamii, hivyo shughuli zingine za kiuchumi zitachukua nafasi, na wanyama wataendelea kupungua na kutoweka. Na hii ni kwa sababu wananchi hawatakuwa na ari ya utetezi wa kiuchumi ili kuwasimamia wanyamapori kwa njia endelevu.

*Kwa kushirikiana na*

policy forum — WILDLIFE CONSERVATION SOCIETY — WWF — PINGO's FORUM — WILDLIFE CONSERVATION SOCIETY OF TANZANIA

*© JMT 2008*

## Nafasi ya wanyamapori katika kupunguza umaskini

Ni muhimu kuhakikisha kuwa wanyamapori wanatoa mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa Tanzania (angalia Chapisho Na. 3). Ni muhimu pia kuwa wanyamapori watoe mchango mkubwa katika kupunguza umaskini na kukuza utajiri katika ngazi ya kijamii. Umuhimu wa kuboresha uhusiano kati ya uchumi wa kitaifa na kupunguza umaskini ngazi ya jamii ndiyo mada kuu katika Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA). MKUKUTA unaahidi jitihada za kuhakikisha kuwa mafao ya ukuaji uchumi yanasambaa hadi vijijini kwa wanajamii na maskini.

MKUKUTA pia unaelekeza mikakati mahususi ambayo itachangia *“michango zaidi kutoka wanyamapori, misitu, na uvuvi na sama kuwaongezea mapato wananchi wa vijijini.”*

Sera ya Wanyamapori ya mwaka 1998 ilitambua umuhimu wa kuongeza mafao ya moja kwa moja kwa wanajamii kutokana na wanyamapori. Lengo la sera lilitamka

*“...jamii na watu binafsi watasimamia wanyamapori katika ardhi zao kwa manufaa yao”* na *“kurudisha majukumu ya usimamizi katika maeneo yanayokaliwa na yasiyokaliwa nje ya maeneo yaliyohifadhiwa kwa wanajamii na sekta binafsi.”*

Sera ya Wanyamapori ya mwaka 2007 inaendelea kutambua ushirikishwaji wa jamii na utoaji wa haki ya kutumia raslimali. Hata hivyo, sera hii mpya iko mbali na uwazi wa kutambua umuhimu wa jamii kupokea mafao kutoka wanyamapori ili kupunguza umaskini na kuanzisha motisha kwa ajili ya uhifadhi wa wanyamapori.

Sera ya mwaka 2007 inafafanua maeneo ya hifadhi za jamii (WMA) kama mfumo wa kulinda makazi ya wanyamapori na kuepukana na uharibifu wa maeneo oevu. Sera inasema kuwa serikali itahakikisha mgawanyo wa haki wa hasara na mafao ambao unajali nafasi ya wadau kutegemeana na makundi ya ardhi na jitihada zilizowekezwa na taasisi katika uhifadhi.Kauli hii inaweza kulinganishwa na sera ya mwaka 1998 ambayo ilisema kwamba jamii watapewa “mamlaka yote” katika usimamizi wa wanyamapori katika maeneo ya hifadhi za jamii (WMA) yaliyo katika ardhi za vijiji.

***Kikwazo kikuu katika kufikia fursa hii ni kwamba tangu wakati wa ukoloni jamii zilizuiliwa kisheria kutumia wanyamapori na haki za kutumia wanyamapori zilibakia na kuthibitiwa na serikali.***

*Kielelezo Na. 1: Mabadiliko katika matumizi ya ardhi katika tambarare za Simanjiro. Je, uchaguzi sahihi wa kiuchumi na kiikolojia unafanyika? Nani anafanya? Nani anafaidika?*



***Kauli nyofu isiyo na mashaka ya kisera* inatakiwa kuwekwa kusaidia utoaji wa haki za kutumia, haki za kusimamia wanyamapori na kubakiza mafao ya kijamii katika ardhi za vijiji kama njia ya kupunguza umaskini, kuongeza utajiri na kuboresha matokeo ya uhifadhi.**

***Kauli nyofu isiyo na mashaka ya kisera* inahitaji kuwekwa kuruhusu uwezekano wa ubunifu na taratibu za usimamizi mbadala kwa jamii ili kusimamia na kupata mafao yatokanayo na wanyamapori katika ardhi za vijiji. Kwa mfano, umiliki wa pamoja wa mahoteli, biashara ndogondogo na kutenga maeneo ya uhifadhi kwa ubia na sekta binafsi.**

***Kauli nyofu ya kisera* inahitaji kutamka uwezo na umuhimu wa jamii katika kusimamia pamoja na serikali maeneo yaliyohifadhiwa - kama ilivyo katika sera ya sekta ya misitu.**

Kama ilivyoelezwa katika Chapisho Na. 3, mwelekeo wa soko wa sasa wa kuongeza uwindaji wa kitalii na utalii wa picha vina uwezo wa kuanzisha fursa za kiuchumi kwa ajili ya wanajamii. Ukweli ni kwamba Tanzania kuna wanyama wengi ukilinganisha na nchi zingine za Afrika, lakini bado maisha ya vijijini (angalia Chapisho Na. 2) nje ya maeneo ya serikali yaliyohifadhiwa ina maana kuwa wanyamapori wana uwezo wa kuzalisha kipato cha moja kwa moja kwa wananchi.

## Maeneo ya Hifadhi za Jamii (WMA)

Sera ya Wanyamapori ya mwaka 1998 ilielekeza mabadiliko ya kisheria yatakayoruhusu uundwaji wa WMA mahali ambapo jamii wangekuwa wasimamizi kisheria na kufaidika na wanyamapori katika ardhi za vijiji.

Katika mwaka 2002 serikali iliunda kanuni za kuongoza WMA, zilizorejewa mwaka 2005, chini ya Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 1974 ambayo inaruhusu uanzishwaji wa maeneo ya hifadhi za jamii katika ardhi za vijiji. Kuanzia Januari 2003 Waziri wa Maliasili ya Utalii amefanya kazi na jamii, Serikali za Wilaya na mashirika binafsi mbalimbali ili kuanzisha maeneo ya hifadhi za jamii yapatayo 16 kwa nchi nzima. Hadi Septemba 2008 maeneo kumi ya hayo yalitangazwa kama WMA, na baadhi ya hayo yalikuwa yameshaingia katika mikataba ya uwekezaji.

Wakati jitihadi zimefanyika katika kuanzisha WMA, matatizo ya kimsingi yamekwamisha maendeleo:

⇨ Awali, kanuni za uanzishwaji maeneo ya WMA ziko changamano na jamii zinahitaji msaada kutoka nje ili kutimiza masharti yote. Hii imehafifisha uanzishwaji wa WMA. Maeneo hayo kama yalivyoanzishwa ni aghali sana kuyaendeleza.



*Kupanga matumizi ya ardhi katika WMA ya Idodi-Pawaga - kukubaliana maeneo ya malisho na yale ya wanyamapori kwa njia shirikishi*

***Moja ya changamoto kubwa ni kwamba kugawana mapato yaliyozalishwa katika maeneo ya WMA hakuko wazi; kanuni zinaeleza tu kuwa mgawanyo wa mafao utaamuliwa kutokana na maelekezo kupitia "nyaraka zitakazotolewa na serikali nyakati tofauti." Kiasi cha maduhuli kutokana na wanyamapori katika WMA hakijawahi kufafanuliwa; Hii inafanya kuwa vigumu kwa jamii kuelewa kama uanzishwaji wa WMA utawaendeleza au la.***

- ⇨ Pili, maeneo ya WMA hayatoi mamlaka ya kutosha kuthibiti mafao ya kiuchumi kwa jamii kutokana na wanyamapori.

## Kufikiria aina mbadala juu ya usimamizi wa wanyamapori kijamii

Zaidi ya WMA kuna njia zingine ambazo jamii zinaweza kupata manufaa ya kiuchumi kutokana na wanyamapori. WMA zimeanzishwa kutoa haki kwa jamii juu ya matumizi ya wanyamapori lakini pia utalii usio wa uvunaji waweza kufanyika katika ardhi za vijiji ambako WMA hazijaanzishwa, kwa vile utalii wa kupiga picha hauvuni wanyamapori.

Kaskazini mwa Tanzania, vijiji vimeingia katika mikataba na wawekezaji ili kuendesha utalii ambao utaleta faida kwa jamii kutokana na wanyamapori.
Mingi ya mikatabi hii ya vijiji na wawekezaji iko katika vijiji kuzunguka hifadhi za Serengeti and Tarangire, na imekuwepo kwa zaidi ya miaka 10 hadi 15 iliyopita. Kumekuwepo na mawakala mbalimbali wa serikali ambao wamesaidia kusukuma jitihada hizo.

*Mathalani:*

- ⇨ TANAPA wamesaidia kijiji cha Ololosokwan kando kando ya Hifadhi ya Serengeti kuanzisha makambi ya kiutalii ili wanajamii waweze kupata mafao ya ziada kutokana na utalii wa wanyamapori. Tangu mwishoni mwa miaka 1990 mapato ya kijiji cha Ololosokwan na vijiji vingine katika Tarafa ya Loliondo (Wilaya ya Ngorongoro) yameongezeka kufika zaidi ya dola za kimarekani 300,00 (TZS milioni 360) kila mwaka kutokana na biashara ya utalii.

Mwenendo wa masoko umesaidia jamii nyingi, kama vile vijiji vya Loliondo kuongeza mapato kutokana na utalii, kwa vile idadi ya watalii wanaokuja Tanzania imeongezeka.

Hata hivyo, jitihada hizi zimekabaliwa na changamoto nyingi. Shughuli za kiutalii katika maeneo haya zimesababisha migogoro na makampuni ya uwindaji yenye vitalu maeneo hayo hayo, hivyo kuweka mafao ya jamii katika hatari. Wawindaji adilifu wamehisi wamelazimishwa kubeba gharama za kuendesha vitalu vya na kwamba makampuni ya utalii wa kupiga picha wamefaidika isivyo halali kutonana na uwekezaji wao. Taratibu mpya zimeanza kuandaliwa kati ya

*Kielelezo Na. 2: Kuongeza mapato kutoka utalii usio wa uvunaji kwa vijiji saba Tarafa ya Loliondo na kwa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro, 1996-2007.*




*Chanzo:Wawekezaji wa Loliondo*

waendeshaji wa makampuni ya uwindaji wa kiutalii na yale ya utalii wapicha, ili kuona namna ya kugawanya hasara na faida za uendeshaji maeneo hayo kwa haki. Na hivyo kuboresha mafao ya jamii. Hata hivyo, kanuni za utumiaji wasio wa kuvuna wanyamapori zilizotolewa mwaka 2007 zinahitaji malipo makubwa kwenda Idara ya Wanyamapori kutoka makampuni ya kiutalii yanayofanya kazi ya utalii katika maeneo hayo. Malipo kama yalivyoelezwa katika kanuni, yatapunguza fedha kwa kiwango kikubwa ambazo makampuni ya kiutalii yanatakiwa kulipa vijijini. Hii itapunguza motisha kwa vijiji kutenga ardhi kwa ajili ya wanyamapori.

Masuala haya ya kugawana mapato kwa sasa yanajadiliwa na wadau mbalimbali na Idara ya Wanyamapori kama yalivyojadiliwa katika Chapisho Na. 3.



*Wavulana wa kihadzabe wakikagua nyayo: Wanyamapori pia huwakilisha thamani ya kijamii na kiutamaduni isiyo na mbadala – baadhi yake zina zaidi ya miaka 40,000*